SautiElimu

hakielimu

Toleo la 14
2006
ISSN 1821 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org



Wanaharakati, nasisi tucheze

Na Fausta Musokwa, HakiElimu

Kwa nini tunajadili suala la michezo? Sababu kubwa ni kwamba huwezi kuongea kuhusu elimu bora bila kutaja michezo. Wataalam wa elimu wanasema michezo pia ina nafasi yake katika elimu kama masomo mengine, kwa mfano hisabati au jiografia.

Kucheza pia ni kujifunza. Ndiyo maana mwaka huu tumemuona Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Margareth Sitta akiahidi Bungeni kwamba wizara yake pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo zitashirikiana kufufua na kuimarisha michezo shuleni.

Wengi tumefurahishwa na tamko la waziri tukikumbuka kwamba hapo nyuma michezo iliondolewa mashuleni. Lakini, tunatumiaje fursa zinazotokana na mabadiliko haya? Tunawapa nafasi watoto wetu kushiriki? Tunaheshimu viwanja vilivyotengwa kwa michezo katika jumuiya zetu?

Kwa mujibu wa wataalam, mshiriki mzuri katika michezo anafaidika kwa namna nyingi. Kwa mfano, anajifunza kujiamini na kupima uwezo wake kwa kushirikiana na watu wengine. Lakini faida haziishii kwake tu. Huyu mtu akitumia kile alichojifunza katika michezo, anaweza kuwa mwanaharakati wa maendeleo katika jumuiya yake. Atakuwa mtu asiyeogopa kuongea na kufuatilia viongozi wake au kushirikiana nao.

Kwa mwanaharakati, michezo inapowaleta watu mbali mbali pamoja kwa furaha, anajua kwamba hapo hapo anaweza kuanzisha mjadala na wale waliokusanyika. Je, wanaharakati wa Marafiki wa Elimu tunafanya hivi?

Kwenye jarida hii la SautiElimu tunakumbushana kuhusu nafasi ya michezo katika jamii yetu. Mathalan, Newton Kyando anaeleza zaidi kuhusu michezo inavyochangia kuiimarisha misingi ya jamii bora. Anaonesha kwamba katika kucheza tunajifunza kanuni za demokrasia, utawala wa sheria na mengineyo.

Naye Mch. Joseph Shakato anatuambia kwamba kucheza ni haki ya watoto na serikali ina wajibu wa kutoa vifaa na kutenga viwanja vya michezo. Anasema: 'Upo umuhimu kwa wazazi, jamii na waelimishaji kujua kuwa ni jukumu letu kuwatia moyo watoto katika suala la michezo.'

Herman J. Magoti anashauri jamii ithamini vipaji vya michezo kwani inaweza kuleta ajira.

Na wewe unasemaje?

Kucheza kuna umuhimu

Na Mch. Joseph Shakato, K.K.K.T Dodoma

Watu wanapofikiri kuhusu haki za watoto, hali ya kucheza si kitu cha kwanza katika mawazo yao. Lakini kucheza ni muhimu sana. Kucheza kuna faida ya kimwili na kiakili katika maendeleo ya kukua kwa mtoto.

Kucheza kunawafanya watoto wajue tabia zinazofaa na zisizofaa, kama kubabaishana. Vilevile, kucheza kunawafundisha watoto kuhusu wanavyoweza kushiriki katika shughuli za burudani na kuwafanya wawe wagunduzi. Pia kunawapa changamoto ya kutumia uwezo wao kimwili. Michezo huupa mwili mazoezi na kuujenga vyema.

Kama ambavyo Mheshmiwa Rais Jakaya Kikwete amelipa umuhimu suala la michezo kwa ujumla, kuna umuhimu wa kufufua michezo katika shule. Pia pawepo na waalimu watakao shughulikia na kusimamia michezo.

Upo umuhimu kwa wazazi, jamii na waelimishaji kujua kuwa ni jukumu letu kuwatia moyo watoto katika suala la michezo. Serikali iwajibike kutoa vifaa na kutenga maeneo ya viwanja vya michezo.

Pamoja na michezo kuwa sehemu mojawapo ya mazoezi ya mwili na kujenga afya kwa watoto, pia inawawezesha kupata mafanikio na kujifunza mengi kwa manufaa ya mchezaji na taifa.

Tutambue kuwa ili kuibua vipaji vya watoto, tuwape nafasi ya kutosha katika michezo.

Wizara husika itilie maanani suala la michezo shuleni.

Je, unayafahamu haya?

Na Newton Kyando, HakiElimu

Michezo ni muhimu mno. Ina jenga afya na ni tiba mbadala lakini zaidi ya hapo, huchangia kuiimarisha misingi ya jamii bora kama ifuatavyo:

Utawala bora: Washiriki huelewa dhana ya uongozi kama uwakilishi na sio usimamizi wala utawala. Katika michezo, timu hupaswa kushirikiana kujua mahitaji yao na pia kuwa na mwakilishi wao atakayeweza kuwakilisha mawazo na matatizo ya timu.

Ushirikiano: Katika shindano lolote la michezo, ushindi ndio lengo la kila upande. Kila upande huandaa mikakati itakayojumuisha nguvu za kila mshiriki. Haya hufanikiwa kuzingatia ufahamu wa washiriki kuwa kwa pamoja ushindi unawezekana na juhudi za wachache hazitazaa matunda kama hamna ushirikiano.

Demokrasia: Kukubali kushindwa ni moja ya utamaduni unaoendelezwa vema na michezo. Anayeshindwa anapaswa kukubali kushindwa na kumpongeza mshindi. Mshindi pia anapaswa kutombeza aliyeshindwa. Anatakiwa kumpongeza kwa jitihada aliyoonesha hasa ushindani bora na umahiri aliouonesha na kwa mchezo wa kuvutia.

Utawala wa sheria: Kila mchezo una sheria na taratibu zake. Hizi zinapaswa kufuatwa ili mchezo uweze kufurahiwa na kufurahisha watazamaji pia. Taratibu kama za 'fair play' zinalenga kuimarisha nidhamu ya wachezaji. Zina wajulisha wachezaji juu ya hatua za kuchukuliwa iwapo taratibu hazikufuatwa. Matumizi ya onyo, adhabu ndogo na kubwa hufuata aina ya kosa, sehemu kosa lilipotendewa na ukubwa wa kosa. Hii ni sawa na mifumo yetu ya kijamii na kisheria pia.

Utu na Haki za Binadamu: Mwanamichezo anahimizwa kujali afya yake kadhalika za wenzake. Utu hujengwa pale mchezo unaposimama kwa vile tu mmoja wa wachezaji ameumia. Hii inajenga hisia sahihi na thabiti ndani ya wanamichezo kuwa bila watu michezo haitawezekana.

Michezo mashuleni ni njia bora na rahisi ya kubadili fikra za wanafunzi kuwa wanajamii wanaojali.

Tudumishe michezo ndani na nje ya shule zetu kujenga jamii bora!

SautiElimu

Toleo la 14
2006
ISSN 1821 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Barua kwa SautiElimu

Hii pia ni njia ya kuingiza kipato

Na Herman J. Magoti, Singida

Michezo ni moja kati ya vitu ambavyo huchangamsha, huburudisha, hufikirisha, hujenga mwili na pia huwafanya watu wawe na mahusiano mazuri na kufahamiana. Pia katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia michezo imekuwa ni sehemu moja wapo ya kujiingizia kipato au ajira.

Kwa maoni yangu kuna umuhimu wa kuwepo michezo shuleni kutokana na sababu zifuatazo:

Kama tujuavyo, samaki mkunje angali mbichi. Kwa hiyo ni muhimu pia kukuza kipaji cha mtoto angali bado mdogo, akiwa shuleni na wala sio kusubiri hadi amalizapo masomo. Ndiyo maana huwa tunakosa wanamichezo wa kuliwakilisha vyema taifa kwenye mashindano mbalimbali.

Sidhani kama michezo inachangia kutofaulu kwa wanafunzi au kushuka kwa taaluma. Michezo ni ajira na watu tunatofautiana katika hali mbalimbali mfano, kuna mwingine hana uwezo wa kukaa darasani kusoma hadi kupata shahada, lakini ana kipaji cha kuchonga, kuchora, kucheza mpira na michezo mingine mbalimbali.

Kwa hivyo tukiwazuia hawa kukuza vipaji vyao huoni kuwa maisha yao ya baadae yatakuwa duni kutokana na kutokuwa na taaluma iliyokamilika hasa kama hawakuwa na uwezo mzuri katika masomo mengine?

Watu wanapokutana katika michezo huwa kuna wataalamu mbalimbali ambao wanahudhuria hapo na hivyo huwapa wale wanaocheza mbinu mbalimbali za kuwasaidia kukuza vipaji vyao au hata kuwatafutia ajira.



Tuthamini maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo

Na Mussa A. Gunda, Singida

Natumia fursa hii kutoa maoni yangu juu ya suala la michezo kwa wanafunzi wa shule za msingi. Nikiwa mmojawapo wa wanamichezo, kwa kweli kwa sasa michezo mashuleni inazidi kufifia siku hadi siku ikilinganishawa nakipindi cha miaka ya nyuma.

Kwa ujumla kipindi cha nyuma, hasa yalipokuwepo mashindano ya UMTASHUMTA, yalipokuwa yanapokaribia watoto walikuwa wakijiandaa na kushiriki kikamilifu ipasavyo kwenye michezo mbali mbali. Viwanja vilikuwa vingi vilivyowawezesha watoto kucheza kwa uhuru. Sasa, hali imebadilika na viwanja vimevamiwa kwa ujenzi wa majengo ya shule na nyumba za walimu.

Suala kama hili lazima liangaliwe upya ili watoto wapate fursa ya kufurahia michezo wakiwapo shuleni.

Michezo ni nguvu na nguzo ya watoto katika kujifunza na kuonyesha vipaji vyao. Hivyo ni wajibu wa jamii kuthamini maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo ili kuwawezesha wanafunzi kupata haki yao ya kucheza.

Tumia kamati za shule kuinua kiwango cha michezo mashuleni

Na Davis Makundi, Dodoma Mjini

Ni wazi kuwa michezo ni urafiki na udugu. Michezo hujenga ujirani na urafiki wa karibu zaidi katika jamii.

Michezo pia huboresha afya. Mashuleni, huongeza hata idadi ya mahudhurio ya wanafunzi, jambo ambalo linakuza kiwango cha taaluma katika shule.

Kutokuwepo kwa michezo mbalimbali mashuleni kunachangia ukosefu wa uhusiano na upendo kati ya wanafunzi na wanafunzi na kati ya shule moja na nyingine kukiwa na shindano la michezo.

Kutokana na umuhimu huo nawasihi na kuwashauri viongozi wa shule kupitia kamati za shule kuhakikisha kuwa suala la michezo linapewa kipaumbele na kutekelezwa kwa vitendo.

Ili kufanikisha suala hili nashauri kamati za shule, na pia walimu, wanafunzi na jamii kwa jumla washirikiane katika kupendekeza michezo inayoweza kuwepo shuleni hasa kulingana na mazingira na uwezo wa shule.

Msingi bora wa utawala ni ushiriki. Hivyo kuwapa nafasi wanafunzi kupendekeza aina ya michezo wanayoitaka kutaongeza ari na tija katika suala la ushiriki wao katika michezo husika.

Tukishirikiana tutaweza.

HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki na demokrasia katika elimu na jamii. Tunafanya hivyo kwa kuwezesha jamii kupata habari, kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera; kuchochea ubunifu wa mijadala ya umma; kufanya utafiti yakinifu, uchambuzi wa sera na utetezi na kushirikiana na wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Shukrani kwa PANOS kwa picha na kwa wote walioandaa habari zilizochapishwa katika jarida hili.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya jarida hili kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chazo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala mbili kwa HakiElimu.

Mhariri Mkuu:
Rakesh Rajani

Timu ya SautiElimu
Robert Mihayo
Fausta Musokwa
Maria Kalavo
Newton Kyando

Tuandikie!

HakiElimu SautiElimu
S.L.P. 79401
Dar es Salaam Tanzania
Simu: 022151852 au 3
Fakisi: 022152449
Baruapepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

ISSN 1821 5076

© HakiElimu 2006

Pata nakala yako ya machapisho yetu mapya. Tuandikie!

Ukurasa wa 2